**<u>Kikao cha dharura cha kamati za Tanden 19.4.2014 Skaffervej 8.1 2400 kbh NV:</u>**

**Walio udhuria kikao:**

1. John Butondo “Mwenyekiti”
2. Dulla Mnanga “Mwenyekiti wa kamati ya Utamaduni”
3. Tambwe “Mweneyekiti wa kamati ya fedha
4. Godfrey Moses
5. Anil Nanji

**Walio toa hudhuru:**

1. Mwesiga
2. Fortunatus
3. Jovin
4. Fadya

**Agenda za kikao:**

1. Tathmini ya sherehe ya Muungano
2. Sherehe zinafuatia( Summer party)
3. Miradi ya Tanden
4. Mengineyo

1. **Tathmini ya sherehe ya Muungano:**
   Mweka hazina aliwarudishia baadhi ya watu walio leta stakabadhi kwaajili ya malipo yao, ya matumizi kwaajili ya sherehe sikiu ya sherehe.( John alieleza hili).

   Kutokana na lengo la sherehe ya uhuru, ya kwamba nia ni kukutanisha waTanzania na marafiki zao na watu kujuana, Kiasi cha pesa kilichopatikana ni 1500kr, ila Mweka hazina atatoa taarifa kamili ya mahesabu.

   John alieleza pia, kuna baadhi ya vinywaji vimebaki kutoka kwenye sherehe ya muungano. John alilisisitiza pia hasara haikupatikana kwani, lengo kama lilivyoelezwa hapo juu ni kukutanisha watu.

2. **Sherehe ya Tanden summer party itakayofanyika Vanløse 07.06.2014**
   Wajumbe wameridhia kwamba summer party ifanyike, licha ya kwamba kutakuwa na sherehe nyingine ya Kikundi cha waKenya waishio hapa kufanya sherehe siku hiyo.

   Wajumbe walizungumzia na kuridhia mambo yafuatayo:
   - Summer party itafanyika na lengo kuu litaelekezwa kwa watoto na utamaduni

- Dulla Mnanga kushirikiiana na John Butondo na Jovin watatuma email kwa wanachama wote(Hususani wazazi), wa Tanden na marafki zao, kuwataka wawaorozeshe watoto wao, ili wajisajili kwaajili ya kushiriki kwenye party.Hii inatakiwa kufanyika haraka iwezekanavyo.

- Dulla amepewa jukumu la kuongea na Said( muwezeshaji wa ngoma za watoto), ili waje na watengeneze ratiba ya watoto siku hiyo. Pia Said aweze kuwashawishi wateja wake ili waweze kujiunga na party ya Tanden ya siku hiyo.

- John na Dulla Pia wataongea na wawezeshaji ( Makungu,na kulwa ) kwaajili ya ratiba ya watoto pia, ili waje kuwezesha siku hiyo.

- Ili sisitizwa kuwekwa video( matangazo) yanayohamasisha wazazi na watoto kuhusu party yetu. Dulla ataongea na Said jinsi ya kupata video za matangazo, Tambwe atatafuta video za Tanden za watoto wakiwa kweneye ngoma n.k , ili kuweka kwenye mitandao ya Tanden.

- Siku ya party kutakuwa na (Hip pop Dance- Tambwe atashughulikia suala hili, Utamaduni na michezo- Dulla,Said, Makungu,Kulwa. Nafasi ya watoto au hata watu wazima kuonyesha viapaji vyao,kuimba,kufokafoka,kucheza n.k kutakuwa na wakati wao. Dulla ataimba na playback kushirikisha washiriki.

- Dj wa siku hiyo watakuwa Anil na Davis ( Davis anatakiwa atengeneze vipeperushi vya sherehe mapema iwezekanavyo, kwani habari zote kuhusu party tayari zimeshapatikana (Ukumbu, kiingilio,muda, vyakula na michezo pamoja na muziki)

- Watu watakao jitolea/kulipwa kwa kutengeneza chakula cha siku ya party watafutwe mapema kuanzia sasa, jukumu hili ni la wote ila litaongozwa na Jovin,Mwesiga,Godfrey na Lilian.

3. **Miradi ya Tanden:**
   Wajumbe wa kikao waliongelea na kujadili kuhusu miradi ya Tanden na yafutayo ndio yalioridhiwa na wajumbe:

   - Watoto waliokuwa wanafadhiliwa na Tanden wameshamaliza masomo ya kiwango cha elimu ya sekondari na hawajabahatika, kuendelea na masomo. Hii imetokana na

uwezo mdogo wa watoto hao. Tanden inabaidi itafute watoto wengine walio kosa nafasi ya kuendelea na masomo lakioni hawana uwezo wa kujilipia.

- Dondoo na ufuatiliaji wa habari za mradi wa Kibiti hospital unahitajika kufuatiliwa, kwani mpaka sasa hakuna habari yoyote kuhusu maendeleo kutoka kibiti.

- Tanden iliomba pesa toka kwa wafadhili hapa Denmark na imepata kiasi cha pesa 7000kr. Wajumbe waliridhia ununuzi wa wa vifaa vya hospitali kwa kushirikiana na NIMR Tanzania, katika mkoa wa Mwanza. Kuna takiwa kununuliwa vifaa viwili Ulta sound machine na Biochemistry machine. Makubaliano ni NIMR watachangia nusu ya pesa 3000$ na Tanden watachangia 3000$ ili kupatikana kwa vifaa hivyo.

- Tanden itaongezea 5000kr kwenye pesa ilizoomba kwa wafadhili ili kuweza kununuliwa kwa kifaa kimojawapo kati ya viwili vilivyotajwa. NIMR watatakiwa kutoma invoice ya malipo kuhusu viufaa hivyo. Suala hili litafuatiliwa na John pamoja na Jovin.

**Mengineyo:**

John aliongelea suala la mbunifu kutoka Tanzania na kikundi chake asilia/Mavazi (Diana Magesa), kwamba kutokana na kutokuwepo kwa muda wa wao kuja kipindi cha summer, basi liangaliwe uwezekana wa wao kuja kwenye sherehe ya mwezi wa nane ( Tanden family day au sherehe ya uhuru). Ufuatiliaje wa viza zao uanze mapema. Ila wanachama inabidi watumiwe link inazoonyesha kazi za Mbunifu Diana.

Lilitolewa pendekezo toka kwa wajumbe ya kufanyika kwa Tanden family day " ifanyike nje, wanachama wasilipie vyakula ,ila marafiki zao watatakiwa kulipia.

Wajumbe walishauri kuongeza nguvu kwenye kamati ya kutafuta pesa Tanden, ili iweze fanya kazi kwa ufanisi. Pia wajumbe walishauri kutafutwa kwa makampuni ili waweze kusaidia sherehe za Tanden.

Wajumbe waliadhiria kuwepo na habari mapema kwa watu watakao shiriki katika kufunga uukumbi baada ya sherehe kuisha , kwani imezoeleka kwa watu wachache kuwa wanafanya kazi hiyo siku zote. Wajumbe walisisitiza kuwepo na habari mapema ya majukumu kwa wanachama katika kushiriki katika sherehe za Tanden.

Link za kazi za mbunifu Diana Magesa ni hii

https://docs.google.com/file/d/0B14N0KhRAlG8dVFaaHFvRzcwZm8/edit?pli=1

John alifunga kikao
Kikao kingine kitaitishwa baada ya pasaka, kwaajili ya utekelezaji wa maadhimio ya kikao.